# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

Februari 2015

# MUHTASARI WA TAMKO LA SERA YA FEDHA

*Mapitio ya Nusu Mwaka*

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**

Februari 2015

## Utangulizi

Taarifa hii ya mapitio ya Tamko la Sera ya Fedha inatathmini mwenendo wa utekelezaji wa sera ya fedha katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2014/15 na kuainisha mwelekeo wa kisera ambao Benki Kuu inakusudia kuchukua katika kipindi kilichobakia cha mwaka wa fedha 2014/15.

## Mwenendo wa Uchumi wa Dunia

Hali ya uchumi wa dunia imeendelea kuwa ya kuridhisha hasa kutokana na kuimarika kwa uchumi wa Marekani na Uingereza kulikochangiwa na kuimarika kwa mahitaji binafsi ya ndani (*private demand*). Ukuaji wa uchumi katika mataifa yanayoibukia kiuchumi (*emerging market economies*) uliendelea kuwa thabiti, ingawa kumekuwa na tofauti kati ya nchi na nchi. Kulingana na Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Januari 2015, uchumi wa dunia unatarajiwa kuongezeka kutoka wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2014 hadi asilimia 3.5 mwaka 2015.

Kupungua kwa kasi ya upandaji bei ya mafuta na bidhaa nyingine kumechangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa mfumuko wa bei katika nchi nyingi duniani tokea mwezi Julai 2014. Nchini Marekani, mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 2.1 mwezi Juni 2014 hadi asilimia 0.8 mwezi Desemba 2014, kutokana na kushuka kwa bei za nishati. Katika nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya, mfumuko wa bei ulishuka chini ya kiwango cha sifuri (*deflation*) wakati ule wa Uingereza ulibaki chini ya lengo la asilimia 2. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei nchini China ulishuka kutoka asilimia 2.3 hadi asilimia 1.5 kutokana na kushuka kwa bei za vyakula.

## Mwenendo wa Uchumi Tanzania

### Tanzania Bara

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2014, uchumi uliendelea kuimarika na kukua kwa asilimia 7.1 ikilinganishwa na makisio ya ukuaji wa asilimia 7.2 kwa mwaka 2014. Kiwango hiki cha ukuaji wa uchumi kilitokana na hali nzuri ya hewa na kuongezeka kwa matumizi ya pembejeo na hivyo kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo. Ukuaji wa uchumi ulichangiwa pia na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani sanjari na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani na nje ya nchi. Shughuli nyingine zilizochangia ukuaji wa uchumi ni pamoja na usafirishaji na mawasiliano, biashara za jumla na rejareja, upangishaji majengo. Uchumi unatarajiwa kuendelea kuimarika katika kipindi kijacho kutokana na uwekezaji unaoendelea katika miradi ya miundombinu, kuongezeka kwa uzalishaji viwandani na huduma nyingine. Marekebisho yaliyofanywa hivi karibuni katika ukokotoaji wa Pato la Taifa kwa kutumia kizio cha mwaka 2007 badala ya 2001 yanaonesha mabadiliko katika muundo na mchango wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa. Matokeo ya marekebisho hayo yanaonesha kuwa mchango wa sekta ya kilimo umepungua wakati mchango wa sekta nyingine rasmi, kama viwanda na huduma za kibenki, umeongezeka.

Mfumuko wa bei umeendelea kupungua hadi kufikia asilimia 4.8 kwa mwaka ulioishia mwezi Desemba 2014, ikiwa ni chini kidogo ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0. Hii ilitokana na hali nzuri ya hewa katika ukanda wa Afrika Mashariki iliyopelekea kuwepo kwa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani na nchi jirani. Aidha, utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha pamoja na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia vilichangia kupungua kwa mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei

usiojumuisha chakula na nishati (*core inflation*) umebaki kuwa katika kiwango cha takriban asilimia 3 katika kipindi chote cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2014/15. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa sanjari na lengo la muda wa kati la asilimia 5, kufuatia kuwepo kwa chakula cha kutosha nchini na kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Takwimu za mapato ya Serikali Kuu zinaonesha kuwa katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2014/15 mapato yalikuwa shilingi bilioni 5,240.6 sawa na asilimia 86.9 ya lengo. Hali hii ilichangiwa na kupungua kwa bidhaa na huduma kutoka nje zinazotozwa kodi, pamoja na kuchelewa kutekelezwa kwa hatua za mapato zilizotangazwa kwenye bajeti ya 2014/15. Matumizi ya serikali yalikuwa shilingi bilioni 6,694.9 sawa na asilimia 78.4 ya makisio, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 4,484.5, sawa na asilimia 78.4 ya makisio. Mapato ya ndani yalikuwa zaidi ya mahitaji ya kugharamia matumizi ya kawaida. Kuanzia mwezi Julai 2014, Serikali imekuwa ikigharamia matumizi ya maendeleo kwa mikopo kutoka soko la dhamana za Serikali pamoja na mapato ya ndani.

Katika kipindi cha miezi mitano ya kwanza ya mwaka wa fedha 2014/15, nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nje, ilipungua na kufikia dola za Kimarekani milioni 1,999.7 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Kimarekani milioni 2,575.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2013/14. Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje, hususan mafuta na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za viwandani katika soko la nje.

Kufikia mwishoni mwa Desemba 2014, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Kimarekani milioni 4,388.6, ambazo zinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.2

(ukiondoa bidhaa na huduma ambazo zinalipiwa na fedha za uwekezaji wa moja kwa moja). Rasilimali za fedha za kigeni za mabenki zilifikia dola za Kimarekani milioni 760.6 mwishoni mwa mwezi Desemba 2014.

Deni la nje liliongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 13,195.6 mwishoni mwa Desemba 2013 na kufikia dola za Kimarekani milioni 14,126.8 mwishoni mwa Desemba 2014 hasa kutokana na mikopo mipya. Wakati huo huo, deni la ndani la serikali liliongezeka kwa asilimia 23.8 hadi shilingi bilioni 7,481.7. Ongezeko hili lilitokana na mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Benki zimeendelea kutumia njia mbalimbali katika kutoa huduma ili kuwafikia wale ambao hawakuwa katika huduma za kibenki. Hali hii imechangia kuongezeka maradufu kwa amana za watu binafsi katika mabenki kutoka ongezeko la shilingi bilioni 1,091.5 kwa mwaka ulioishia Novemba 2013 hadi ongezeko la shilingi bilioni 2,174.2 kwa mwaka ulioishia Novemba 2014. Tathmini ya Takwimu za hali ya benki nchini kwa mwaka ulioishia Novemba 2014, inaonesha kuwa benki ziko imara na salama na zinaweza kustahimili misukosuko ya kifedha. Mitaji ya benki pamoja na ukwasi vilikuwa asilimia 16.6 na 37.1 kwa mwaka unaoishia mwezi Novemba 2014, ambavyo ni juu ya viwango vilivyowekwa kisheria vya asilimia 10 na asilimia 20, kwa mtiririko huo.

**Zanzibar**

Katika kipindi cha robo tatu za kwanza kwa mwaka 2014, uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 8.5 ikilinganishwa na asilimia 6.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2013. Ukuaji wa uchumi ulichochewa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa uzalishaji wa bidhaa za viwandani, biashara na bima, uvuvi, na shughuli za utalii hasa mahoteli na migahawa.

Mfumuko wa bei uliongezeka kwa asilimia 4.4 mwezi Desemba 2014 ikilinganishwa na asilimia 3.8 kwa kipindi kama hicho mwaka 2013. Hali hii ilitokana na kuongezeka kwa bei katika baadhi ya vyakula, hasa samaki, mchele na ndizi. Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki katika kiwango cha tarakimu moja katika kipindi cha nusu ya pili ya 2014/15 kutokana na kuendelea kupungua kwa kasi ya upandaji wa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2014/15, mapato ya ndani ya serikali yalifikia shilingi bilioni 182.7 sawa na asilimia 94.6 ya lengo. Misaada ilikuwa shilingi bilioni 22.1 na mikopo ya nje ilikuwa shilingi bilioni 21.1. Matumizi yalikuwa juu ya makadirio ya shilingi bilioni 218.0 kwa asilimia 6.4, kutokana na kuongezeka kwa fedha za miradi kutoka nje.

Katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2014, ziada ya urari wa biashara ilikuwa dola za Kimarekani milioni 12.6, ikilinganishwa na ziada ya dola za Kimarekani milioni 14.8 mwaka 2013. Hali hii ilichangiwa na kupungua kwa fedha za wahisani.

**Utekelezaji wa Malengo ya Sera ya Fedha ya Mwaka 2014/15**

***Malengo ya Sera ya Fedha***

Kutokana na mwenendo wa uchumi wa hivi karibuni, malengo yaliyoainishwa kwenye Tamko la Sera la Juni 2014, yamefanyiwa marekebisho yafuatayo:

i. Ukuaji wa Fedha Taslimu (Reserve Money) usiozidi asilimia 15.0 badala ya asilimia 14.0;

ii. Ukuaji wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 15.8 badala ya asilimia 15.5

iii. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi wa asilimia 19.5 badala ya asilimia 16.0

iv. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi bila kujumuisha uagizaji wa bidhaa zinazogharamiwa na wawekezaji kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

***Utekelezaji wa Sera ya Fedha***

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2014/15, hali ya ukwasi kwa ujumla katika mabenki ilikuwa ya kuridhisha. Benki chache zilichukua mikopo ya muda mfupi Benki Kuu na kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni hasa mwezi Julai 2014, ili kukidhi mahitaji yao ya ukwasi. Hali hii pia ilijidhihirisha katika mwenendo wa viwango vya riba katika soko la fedha kati ya mabenki. Riba katika dhamana za serikali zilibakia kuwa juu sambamba na sera ya fedha, wakati riba za amana na mikopo ya mabenki nchini hazikuwa na mabadiliko makubwa.

Ili kuhakisha kuwa hali ya ukwasi inawiana na shughuli za kiuchumi, Benki Kuu ilishusha kiwango cha lazima cha sehemu ya amana za watu binafsi katika mabenki, ambacho mabenki yanatakiwa kuhifadhi Benki Kuu kutoka shilingi 10 hadi shilingi 8 kwa kila shilingi 100 mwezi Desemba 2014. Hatua hii itaongeza ukwasi kati ya mabenki, kupunguza gharama za mitaji na hivyo kushusha riba za mikopo.

Kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) umeendelea kukua kwa wastani wa asilimia 15.2 katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2014, ikiwa ni ndani ya lengo la asilimia 15.8 kwa mwaka wa fedha 2014/15. Vile vile, vigezo vyote vya Mpango wa Ushauri wa Kisera *(Policy Support Instrument)* kwa Desemba 2014 vilifikiwa.

***Mwenendo wa Sera ya Fedha katika Nusu ya Pili ya 2014/15***

Benki Kuu itaendelea kuboresha utekelezaji wa sera ya fedha ili kuhakikisha kuwa kiwango cha ukwasi kinawiana na shughuli za uchumi na kuongeza umuhimu wa riba kutumika kama nyenzo ya mwelekeo wa sera ya fedha.

Kwa kuanzia, Benki Kuu itaruhusu mabenki kutumia amana zao zilizopo Benki Kuu zaidi ya kiwango kilichowekwa kisheria ilimradi mabenki yahakikishe kwamba kwa wastani kiwango kinakidhi matakwa ya sheria ndani ya muda uliowekwa (*maintenance period*). Hatua hii inatarajiwa kuimarisha hali ya ukwasi wa mabenki na hivyo kupelekea utulivu wa riba katika soko la fedha kati ya mabenki, ambao ni moja ya vigezo katika kuelekea kwenye matumizi ya riba kama nyenzo kuu ya sera ya fedha.

## Hitimisho

Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2014, pato la Taifa lilikua kwa asilimia 7.1 wakati mfumuko wa bei ulishuka na kufikia asilimia 4.8 mwezi Desemba 2014.

Shughuli za uchumi zinatarajiwa kuendelea kuimarika katika nusu ya pili ya mwaka 2014/15 zikichochewa zaidi na ukuaji wa uzalishaji wa viwandani, kuendelea kukua kwa sekta ya huduma, hali nzuri ya hewa pamoja na kuimarika kwa uchumi wa Marekani na Uingereza kutakakoongeza mahitaji ya bidha na huduma katika soko la dunia.

Benki Kuu itaendelea na utekelezaji wa sera ya fedha ili kuhakikisha mafanikio ya kiuchumi yaliyofikiwa katika nusu ya kwanza ya 2014/15 yanaendelea na mfumuko wa bei unabaki sanjari na lengo la muda wa kati la asilimia 5.

Ni matarajio ya Benki Kuu kuwa utekelezaji wa sera ya fedha ikisaidiwa na uwianishaji wa mapato na matumizi ya serikali, itaweza kufikia malengo ya sera ya fedha ifikapo Juni 2015 na kuchangia zaidi katika kufikia malengo ya uchumi jumla.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi
Benki Kuu ya Tanzania, 2 Mtaa wa Mirambo, 11884 Dar es Salaam
Simu: +255 22 2233328, +255 22 2233350, Nukushi: +255 22 2234060
Tovuti: http://www.bot.go.tz

Printed by Identity Promotion Ltd